# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA

## BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU TANZANIA (NBAA)

SIMU: +255 26 2963318-9;
NUKUSHI: +255 22 2150648
BARUA PEPE: info@nbaa.go.tz
TOVUTI: www.nbaa.go.tz

4 BARABARA YA UKAGUZI,
"JENGO LA UKAGUZI", GHOROFA YA NANE,
S.L.P. 1271,
41104 TAMBUKARELI,
DODOMA, TANZANIA

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na.:** DE.17/367/01/31 **Tarehe:** 21.12. 2023

## TAARIFA KWA UMMA

Katika kikao cha 193 cha Bodi ya Wakurugenzi ya NBAA kilichofanyika leo tarehe 21.12.2023 kimejadili na kupitisha maazimio mbalimbali. Nachukua wasaa huu kuwajulisha baadhi tu ya maazimio yaliyojadiliwa kwenye kikao hicho hasa yale ambayo ni muhimu kufahamika kwa wadau wetu mbalimbali na umma kwa ujumla.

**Jambo la kwanza: KUPITISHA MATOKEO YA MITIHANI YA 98 YA BODI**

Bodi ya Wakurugenzi imejadili na kupitisha matokeo ya mitihani ya 98 ya Bodi ambayo ilifanyika mwezi Novemba mwaka huu.

**Matokeo ya Jumla**

Watainiwa waliosajiliwa walikuwa **7,238.** Watahiniwa **527** sawa na asilimia **7.3** hawakuweza kufanya mitihani kwa sababu mbalimbali. Hivyo idadi ya watahiniwa waliofanya mitihani hiyo ni **6,711** sawa na asilimia **92.7**. Kati ya watahiniwa walisajiliwa kufanya mitihani watahiniwa **3,636** sawa na asilimia **50.2** walikuwa wanawake na watahiniwa **3,602** sawa na asilimia **49.8** walikuwa wanaume.

Kati ya watahiniwa waliofanya mitihani hiyo watahiniwa **4,468** sawa na asilimia **66.6** wamefaulu mitihani yao ambao kati yao watahiniwa **1,185** sawa na asilimia **17.7** ni wale waliofaulu masomo yote katika ngazi husika na hivyo wanastahili kupatiwa barua za ufaulu na watahiniwa **3,283** sawa na asilimia **48.9** ni watahiniwa

ambao wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi husika. Watahiniwa waliobakia ambao ni **2,243** sawa na asilimia **33.4** walishindwa mitihani yao katika ngazi husika.

Mchanganuo juu ya matokeo hayo yapo kwenye taarifa rasmi ambayo itakabidhiwa kwenu Waandishi wa Habari na pia matokeo yatawekwa kwenye tovuti ya Bodi pamoja na kuingizwa kwenye akaunti ya kila mtahiniwa.

## Jambo la pili: UZINDUZI WA MIHUTASARI MIPYA YA BODI PAMOJA NA VITABU VYA REJEA

**Utangulizi:** Bodi hufanya mapitio ya mitaala yake pamoja na vitabu kila baada ya miaka mitano. Zoezi la mwisho lifanyika mwaka 2019. Bodi inayo mihutasari (syllabi) mitatu ambayo ni Mtaala wa Cheti Ngazi ya Awali (Accounting Technician Level I) ambao una masomo manne; muhutasari wa pili ni wa wa Cheti Ngazi ya Pili (Accounting Technician II) ambao pia una masomo manne; muhutasari wa tatu ni ule wa Ngazi ya Taaluma (Professional Level) ambao una masomo kumi na sita. Hivyo idadi ya masomo katika mihutasari yote mitatu ni ishirini na nne.

**Kazi iliyofanyika:** Bodi ilianza mchakato wa kupitia mitaala yake pamoja na vitabu vya rejea kuanzia mwezi Agosti 2022. Zoezi hili lilianza kwa kufanya marekebisho ya mitaala na baada zoezi la kupitia vitabu vya rejea lilifanyika.

Kazi ya kurekebisha mihutasari ilianza kwanza na zoezi la kuchukua maoni kutoka kwa wadau mbalimbali. Baada ya kukusanya maoni hayo yalichakatwa na kutumika kama nyenzo mojawapo katika zoezi la mapitio. Zoezi la kupitia somo moja baada ya jingine lilifanyika ili kuondoa mada zilizokuwa zimepitwa na wakati na kuingiza mada mpya. Pia mada mpya ambazo hazikuwepo kabisa ziliongezwa. Masomo mengine yaliboreshwa kwa kuongezewa mada za somo jingine. Mfano, somo la Uchumi liliongezewa mada za Kodi na somo la Uhasibu liliongezewa mada za Ukaguzi. Masomo yote haya yapo kwenye Ngazi ya Awali ya Taaluma. Baada ya maboresho ya mihutasari lilifuatia zoezi la marekebisho ya vitabu vya rejea. Zoezi hili lilihakikisha kwamba kila mada iliyopo kwenye Mihutasari inayo notisi za rejea kwenye kitabu.

**Kuanza kutumika:** Bodi imepitisha Mihutasari mipya pamoja na vitabu vya rejea kuanza kutumika kuanzia Januari 2024 ila mitihani ya kwanza kwa kutumia mihutasari hiyo itafanyika mwezi wa Novemba 2024.

**Pongezi:** Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Uongozi mzima wa NBAA unapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wataalamu wote walioshiriki katika zoezi zima la kupitia mitaala yake pamoja na vitabu vya rejea. Bodi itaendelea kutambua mchango wao katika taaluma nzima ya Uhasibu hapa nchini.

**Mwito:** Bodi inatoa wito kwa Watahiniwa wote wa Mitihani ya Bodi waliopo na watakaosajiliwa baadae pamoja na Walimu kutumia mitaala hiyo pamoja na vitabu vya rejea kwa usahihi ili kuongeza ufaulu katika mitihani ya Bodi.

**Mwisho:** Sasa naomba kutangaza kuwa mihutasari mipya ya mitihani ya Bodi pamoja na vitabu vya rejea vimezinduliwa rasmi leo tarehe 21.12.2023.

**Jambo la tatu: SHERIA NDOGO ZA MAFUNZO NA MITIHANI YA WAHASIBU NA WAKAGUZI YA MWAKA 2023**

Sheria Ndogo za Mafunzo na Mitihani (zilizorekebishwa) zilipitishwa rasmi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Julai mwaka 2023. Sheria hizi ndogo zimefanyiwa maboresho kadhaa pamoja na kuongezeka kwa vifungu vingine ambavyo vinaendana na mabadiliko ya Sheria mama (The accountants and Auditors (Registration) Act,Cap 286). Moja ya mambo yaliyorekebishwa ni suala la muda wa kukamilisha ngazi ya mitihani ya Bodi. Sheria ndogo ya zamani(2014) kifungu 4.2 cha Jedwali la Tatu kilitamka kuwa mtahiniwa atamaliza ngazi ya mitihani ndani ya miaka mitatu (mihula 6 ya mitihani). Katika Sheria ndogo hizi zilizorekebishwa kifungu cha 6.2 kimerekebishwa kuwa miaka sita (mihula 12 ya mitihani). Bodi ya Wakurugenzi katika kikao chake cha 193, kwa kuzingatia masharti ya kifungu hicho, kimepitisha yafuatayo:-

- Watahiniwa 397 ambao walistahili kufutiwa matokeo yao baada ya kushindwa kumaliza ngazi za mitihani ndani ya miaka mitatu, hawatafutiwa matokeo yao na wataruhusiwa kuendelea na mitihani kwa muda mwingine wa miaka mitatu kila mmoja kulingana na muda wake wa usajili.

- Kila mtahiniwa aliyekuwa amesajiliwa kwa mitihani ya Bodi kabla ya mwezi Julai 2023 atakuwa anaongezewa miaka mitatu zaidi ya kufanya mitihani pale anapofikia ule ukomo wa miaka mitatu.

Maamuzi haya yamefanyika baada ya kudhihirika kuwa nafasi yao ya mwisho ya watahiniwa 397 ya kufanya mitihani ya Bodi kabla ya kufutiwa, iliangukia mbele baada ya marekebisho ya kanuni hizi (Julai,23) hivyo, kuwafanya kuwa na stahiki ya kuongezewa muda kama watahiniwa wapya.

**Jambo la nne: YAHUSU WAHASIBU WAHITIMU (GRADUATE ACCOUNTANTS) WALIOOMBA KUPANDA KUWA WAHASIBU AU WAKAGUZI WA HESABU (ACPA)**

Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) inapenda kuwajulisha Wahasibu Wahitimu (Graduate Accountants) wote walioomba kupanda daraja kuwa Wahasibu au Wakaguzi wa Hesabu kuwa Bodi ya Wakurugenzi, pamoja na mambo mengine, katika kikao chake cha 193 kimepitisha ombi la kuongeza muda ili kuruhusu Wahasibu Wahitimu kukamilisha maombi yao ifikapo tarehe 15 Machi 2024. Maombi yote ambayo yatakuwa hajakamilika hadi kufikia tarehe hiyo, yatakataliwa na muombaji atalazimika kuanza upya muda wake wa mafunzo kwa vitendo kwa miaka mitatu. Bodi inasisitiza kuwa Wahasibu Wahitimu ambao maombi yao yamerudishwa kwao zaidi ya 500 hadi leo, kwa ajili ya kuyafanyia kazi wayafanyiwe kazi mapema na kuyarudisha Bodi haraka iwezekanavyo. Ikumbukwe kwamba maombi yote ya kupanda daraja yanafanyika kwa njia ya mfumo wa kielektroniki uliowekwa na Bodi na hakuna chombo kingine kinachoweza kufanya majukumu hayo ni Bodi na Mhitimu mwenyewe, hakuna uwakilishi.

**Jambo la tano: DIPLOMA YA KITAALUMA KATIKA UKAGUZI WA NDANI (PROFESSIONAL DIPLOMA IN INTERNAL AUDIT- PDIA)**

Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) inapenda kuwajulisha wadau wake kuwa imeanzisha Diploma ya Kitaaluma katika Ukaguzi wa Ndani katika mwaka huu wa fedha 2023/24. Na hii imetokana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Ndani (International Professionals Practice Framework- IPPF) kutaka

ukaguzi wa ndani ufanywe wakati mwingine na wataalam wa taaluma nyingine ambao sio wahasibu. Hii imesababisha wakati mwingine ukaguzi wa ndani kutofanyika vyema. Hivyo Bodi inalenga kuwasaidia wakaguzi wote wa ndani ambao hawana taaluma ya uhasibu ili wafanye kazi zao kwa ufanisi zaidi. Muda wa kusomea Diploma hii itakuwa ni miezi minne (04). Kozi ya kwanza itaanza mwezi Aprili 2024 na mitihani yake kufanywa mwezi Agosti 2024.

**Kwa pamoja tutaijenga Tanzania yetu.**

**ASANTENI**

**CPA. PIUS A. MANENO**
**MKURUGENZI MTENDAJI**